


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA,
Simu : (027) 2503538/ 2507928,
Nukushi: (027) 2505973,
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

OKTOBA 26, 2020

TAKUKURU KARATU YAREJESHA FEDHA SHILINGI MILIONI 56.7 ZIKIWEMO ZA VITAMBULISHO VYA WAJASIRIAMALI ZILIZOKUWA ZIMEFANYIWA UBADHIRIFU

Ndg Wanahabari,

Tumewaita hapa leo, ili kwa kutumia taaluma yenu ya habari tuweze kuufahamisha umma juu ya jitihada za Mapambano Dhidi ya Rushwa zinazofanywa na ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Karatu mkoani Arusha zinazoenda sanjari na kulinda haki za wanyonge pamoja na kuhakikisha kwamba sheria, kanuni na taratibu za vyama vya ushirika zinafuatwa.

Ofisi ya TAKUKURU (W) Karatu mkoani Arusha, leo tarehe 26.10.2020 inaufahamisha umma kwamba kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2020 imefanikiwa kuokoa fedha jumla ya shilingi Milioni Hamsini na Sita laki Saba na elfu Sitini na Saba, mia Nane Hamsini na Tano (**Sh. 56,767,855/-**). Fedha hizo ni za makundi mbalimbali ikiwemo mapato ya serikali, chama cha ushirika, SACCOS na watu binafsi. Mchanganuo wa fedha hizo zilizookolewa ni kama ifuatavyo;

1. Fedha kiasi cha shilingi Milioni Kumi na Tisa na laki Tano (**Sh. 19,500,000/-**) ni sehemu ya fedha za mauzo ya vitambulisho vya wajasiriamali katika wilaya ya Karatu. Awali ilielezwa kwamba mapato ya

mauzo ya vitambulisho vya wajasiriamali yaliyokuwa benki yalikuwa hayaendani na jumla ya vitambulisho vilivyokuwa vimeuzwa. Baada ya TAKUKURU KARATU kupokea malalamiko haya na kuyathibitisha iliwaagiza wale wote waliobainika kusababisha hasara hiyo kurejesha fedha iliyokuwa imepungua ambapo jumla ya shilingi Milioni Kumi na Tisa na laki Tano (**Sh. 19,500,000/-**) zimerejeshwa.

2. Fedha kiasi cha (**Sh. 2,241,000/-**) ni za ujenzi wa ofisi ya Kijiji cha Kiwanja ambazo zilifanyiwa ubadhirifu na Afisa Mtendaji wa Kijiji hicho na kiasi kingine cha shilingi laki Sita na elfu Ishirini na Tatu (**Sh. 623,000/-**) ni za ujenzi wa sekondari ya Eyasi ambayo nayo ilifanyiwa ubadhirifu na uongozi wa Kijiji.
3. Fedha kiasi cha Milioni moja Laki Mbili na elfu Hamsini na Sita (**Sh.1, 256, 000/-**) ni za AMCOS ya Gilala. Fedha hizi ni ambazo baadhi ya wanachama na viongozi wa chama hicho walijikopesha bila kurejesha kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea na hivyo kuwanyima wanachama wengine nafasi ya kukopa.
4. Fedha kiasi cha jumla ya shilingi Milioni Thelathini na Mbili, Laki Saba Tisini na Tatu, mia Nane Arobaini na Saba (**Sh. 32,793,847/-**) ni za SACCOS ambapo Mng'ola SACCOS itakabidhiwa shilingi Milioni Kumi na Saba, Laki Saba Sitini na Sita Mia Sita Sitini na Saba (**Sh. 17,766,667/-**) na Mbulumbu SACCOS shilingi Milioni Kumi na Tatu Mia Saba Sabini na Moja , Mia Moja Themanini (**Sh. 13,771,180/-**). Fedha hizi ni ambazo baadhi ya wanachama na viongozi wa SACCOS hizo walijikopesha bila kurejesha kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea na hivyo kuwanyima wanachama wengine nafasi ya kukopa.
5. Fedha kiasi cha shilingi Laki Sita (**Sh. 600,000/-**) ni mishahara ya watumishi 3 wa USAFI GROUP waliokuwa wanamdai mwajiri wao. Kampuni hiyo iliwaachisha watumishi hao kazi bila kuwalipa mishahara hiyo ya miezi miwili.

Fedha hizi zote zilizookolewa shilingi Milioni Hamsini na Sita laki Saba na elfu Sitini na Saba, mia Nane Hamsini na Tano (**56,767,855**) zitakabidhiwa kwa wahusika hapa mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Karatu Mh ABAS KAYANDA.

Ndg Wanahabari,

Ofisi ya TAKUKURU wilaya ya Karatu, inatumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi wa Wilaya ya Karatu na Mkoa wa Arusha kwa ujumla, kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu hasa wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao. Pia tunatoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana nasi katika mapambano dhidi ya Rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa kitika ofisi za TAKUKURU.

IMEANDALIWA NA:



Sabas Salehe - 0738 150 064

NAIBU MKUU TAKUKURU (M) ARUSHA